SAUTI ZA WASOMAJI

COASTWEEK Sanduku la Posta 87270, Mombasa KENYA

Viongozi Pwani wacheni mizozo

NIKIWA msomaji maarufu wa gazeti la *COASTWEEK*, najitokeza leo kutoa ombi kwa viongozi wetu wanasiasa washirikiane pamoja katika kazi za ujenzi wa taifa.

Nimelazimika kutoa ombi hili kutokana na migogoro midogo midogo ambayo wanasiasa wetu wa Pwani wanayazusha na kuleta hali ya kutoelewana na hii ndiyo inasababisha kwa mambo mengi ya maendeleo kurudi nyuma.

Kwa wakati huu ambapo Wilaya ya Mombasa inajitayarisha kuchangisha fedha kwa ajili ya mchango wa shule za Maingi, viongozi wetu wanahitajika kusahau tofauti walizonazo na wafanye kazi pamoja ili mkoa wetu uchangishe fedha nyingi za kuvunja rekodi wakati Rais Moi atakapotembelea kuendesha harambee hiyo.

Nampongeza Waziri wa Serikali za Mitaa, Bw. Stanley Oloitiptip kwa juhudi yake ya kuleta usuluhisho wa kuduma kati yake na Bw. John Keen. Mfano huu wa Bw. Oloitiptip unahitajika kuigwa na viongozi wa Pwani wa kufanya masilahi kwa manufaa ya wananchi na maendeleo ya mkoa.

Umefika wakaati kwa viongozi ambao bado wanaekeana dukuduku la moyo na uchukivu kwa mwenzake, aliondowe dukuduku hilo mara na washirikiane kwa maendeleo ya haraka.

Johnson Mwero,
MOMBASA.

• *MNYIKA MWAIGHO*

KILIO CHA WAKAZI WA MWANDA

WAKAZI wa Mwanda wana pata matatizo mwingi sana kutokana kwamba hakuna afisa wa kupima nyama. Watu wanategemea mifugo yao baada ya kuuza lakini sasa haiwezekani kwa sababu hakuna mtu wa kupima nyama.

Nikiwa sababu hiyo hivi sasa watu hawali nyama kabisa katika taarafa hii. Tungeomba serikali iamdike mtu ambaye ataangalia suala hili.

Na pia zahanati ya Mwanda haina madawa kwa miezi mingi hivi sasa na inalazimwa watu na watoto kusafiri hadi Wesu kwa matibabu. Twaomba serikali ifikirie zahanti hii.

Mnyika Mwaigho,
Magongo,
MOMBASA.

HUU NI WAKATI WA WAZAZI NA WANAFUNZI KUJIREKEBISHA

MWAKA WA masoma hapa Kenya umebakiwa na kipindi kimoja pekee kumalizika na hivyo kuwapeleka wanafunzi katika madarasa mapya, kwa kufuzu ama kwa kuvilikiwa. Katika kipindi hichi cha pili kina chomalizika tarehe saba Agosti, kulikuwemo na mtihani wa majaribio, yaani matayarisho ya ule Mtithani wa Kenya nzima wa C.P.E.

Madhumuni ya mtihani huu, ni kuwaandaa wanafunzi wa madarasa ya saba ili waanze kuzoea aina yenyewe ya mtihani na isiwaletee wanafunzi hao kuanza kutetemeka siku ya mtihani. Kadhalika mtihani huu humsaidia mwalimu wa darasa la saba kwa kumkumbusha baadhi ya mambo ambayo hahayafunza. Na mara nyingi hutokea kwamba mwanafunzi anayefaulu katika mtihani huu wa majaribio, basi pia hufaulu katika mtihani wenyewe, na yule anayeanguka, basi pia huanguka katikamtihani wenyewe ila kwa alijipinda na akasawazisha ratiba yake ya kudurusu.

Kwa hivyo huu ni wakati mzuri wa mzazi kumrakibisha mtoto wake baada ya kwisha kuona vile alivyofanya katika huo mtihani wa majaribio. Lakini tabia hii ya wanafunzi kupuuza na kudarisi masomo yao kwa shebaha ya kufanya vizuri zaidi katika mtihani wao haipo hapa Mombasa. Hapa Mombasa, maana ya likizo hapa mjini Mombasa, huchukuliwa kuwa ni wakati wa wanafunzi kucheza madisko, kuanza kumiminika katika vilabu vya usiku kwa wingi, kuchukua mafunzo ya kulewa na kuvuta sigara na kuanza kuingia mitaani kwa mitindo ya mavazi namna namna.

Ubaya wa matendo haya ni kwamba wanafunzi hawa wakati wa kufanya vituko hivi vyote hawachukuliwi hatua yoyote. Na kwa vile wanafunzi huutumia mwezi mzima wa mapumziko katika hali hii ya kuharibu akili zake, basi mara shule zinapofunguliwa, huwa watoto hawa hawakujitayarisha marekibisho yoyote ya elimu. Hivyo wao wao huwa wanataka wamalize huo mwaka ili wakaendelee na maisha ya anasa. Hii ni moja miongoni mwa sababu zinazofanya Wilaya ya Mombasa siku zote ishindwe na Wilaya nyengine katika matokeo ya C.P.E.

Hakuna sababu yoyote ya Wilaya ya Mombasa siku zote kuchukuliwa nanga kwenye matokeo ya C.P.E., maana Mombasa pana natija nyingi za kukuza masomo ya mtoto natija ambazo hazipatikani katika Wilaya nyengine. Lakini watoto huletwa na wazazi ambao wanawapenda sana watoto wao hadi hufikia wakati ambapo mwanafunzi hutoroka shule muda wa wiki tatu ama zaidi, na wakati akirudi, basi mzazi atakuja kumsaidia.

Haya tumeyaona kwa macho yetu, yaani mzazi anampa ruhusa mtoto wake atoroke shule. Sasa mtoto sampuli hino atatarajiwa apate natija gani katika mtihani. Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo. Hatuna budi kuwatanabahisha baadhi ya wazazi wa Mombasa kwamba muna tabia ya kudekeza watoto wenu, na huku kudekezwa ndiko kunakowaharibia maendeleo maskulini.

Mbiu ya mgambo kwa gazeti la Kiswahili kwa Waswahili

Na Abdulrahman Sheriff

WANACHI walio mashabiki na wasomaji maarufu wa magazeti ya lugha ya Kiswahili wanajiuliza ni kwa nini magazeti ya Kiswahili yanashindwa kuishi ama ni sababu gani hasa inayosababisha magazeti hayo 'kufa' kifo kisichotazamiwa.

Kwa hakika, wananchi hao hasa kutoka mkoa wetu wa Pwani hupendelea zaidi kusoma magazeti ya Kiswahili lakini hukosa 'uhondo' siku za Jumapili wakati ambapo hakuna gazeti lolote la lugha hiyo linalochapishwa.

Nchi yetu ya Kenya inathamini sana lugha ya Kiswahili lakini inasikitisha kuona Jumapili wasomaji wa Kiswahili hukosa upumbazi ambao wasomaji wenzao wa magazeti ya Kiingereza huupata siku hiyo.

Kulikuwako gazeti moja lilijitokeza kila Jumapili na likawa maarufu kwa wasomaji wa Kiswahili waliofurahikia kuanzishwa kwake. Lakini liliwapa pigo kubwa kwa wasomaji wake liliposhindwa kujihami na likatoweka 'ghafla' bila ya kutegemea.

Matangazo

Sababu kubwa iliyoelezwa na Wakurungenzi wa gazeti hilo wa kulifunga gazeti hilo ni kwamba walikosa matangazo ya biashara; matangazo ambayo ni kawaida kwa gazeti lolote kuyapata katika kujiendeleza na kujipatia faida.

Likajitokeza gazeti lingine lilojaribu bahati yake lakini nataraji kutoweka kwa kukosekana kwake kila wakati kumetokana na ukosefu wa matangazo ya biashara. Ingawa wafanya kazi wa magazeti ya Kiswahili wanajitahidi kuyapata matangazo, hushindwa kuyapata na mwishowe huwa hakuna la kufanyika ila kuliua gazeti.

Litakuwa jambo la busara ikiwa Serakali yetu tukufu inayosisitiza umuhimu wa lugha ya Kiswahili itafikiria kuanzisha gazeti la Kiswahili angalau litoke siku za Jumapili. Gazeti kama hilo halitopata shida ya matangazo kwani Wizara na Idara mbali za Serakali zitatoa matangzo na kusaidia kuendesha gazeti kama hilo.

Ama ikiwa watu binafsi watajitokeza kuanzisha gazeti la Kiswahili, basi mashirika ya Serakali yangelijitokeza kusaidia kwa kutoa matangazo ili wanachi wasomaji wa Kiswahili wapate kuyasoma na kujua kama kuna nafasi za kazi ambazo waweza kuzifanya wapate kufanya maombi.

Umefika wakati kampuni zinazosimamia magazeti zifanye taratibu za kuanzisha gazeti la Kiswahili kwa siku za Jumapili ili wananchi wanufaike kwa habari moto kutoka nchini na Ulimwenguni badala ya kuwekewa habari hadi Jumatatu ambapo ladha yake huwa imeshatoweka.

BALOZI WA OMAN AZURU PWANI

MMOJA KATIKA watu mashuhuri wa Nairobi walioteremkia huku Pwani kusherehekea Sikukuu ya Idd-ul-Fitr alikwa Balozi wa Oman, Mheshimiwa Sheikh Abdulla Said Abdulla.

Mheshimiwa Sheikh Abdulla alisali sala ya Iddi katika Msikiti wa Ibadhi mjini Mombasa. Baada ya sala na kutoa mkono kwa Waislamu waliofika kusali pamoja naye, aliruka kwa ndege mpaka Malindi na Lamu ambako alitoa zawadi za Qurani Takatifu katika misikiti yote ya miji hiyo kwa niaba ya Wizara ya Auqaf ya Oman.

Aliporudi Mombasa, alizuru Masjid Baluchi ambako pia alitoa nakala chache za Qurani. Alipokewa na Imamu wa msikiti, Mullah Abdulrasul Tajadin; Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wabaluchi, Haji Adam Suleiman; Katibu wa Jumuiya Maalim Mohamed Kamal Khan, na Mzee wa Kibuluchi, Sheikh Sood Suleiman Mirza.

MSIKITI WA TABAKA ZOTE

Sheikh Sood alimshukuru Balozi huyo kwa zawadi yake na akamuomba ambaleghesheе Sultan Qaboos wa Oman salamu nyingi za heri kutoka kwa Waislamu wote wa Jamhuri ya Kenya. Na Maalim Kamal Khan akaongeza kwa kusema hakuna zawadi bora kuliko Qurani ambayo imekusanya Maneno ya Mwenyezi-Mungu; ni zawadi yenye kuleta baraka kwa wale walioitoa na wale walioipokea.

Mheshimiwa Sheikh Abdulla katika jawabu yake aliwasifu Wabuluchi kwa kujenga msikiti wa kupendeza sana unaosaliwa na Waislamu wa tabaka na jinsi zote.

Mwisho akasema kuwa Kenya na Oman zina urafiki mkubwa sana na kuwa nchi hizi mbili zimekuwa na fungamano la kihistoria kwa karne nyingi.

WANABAHARIA WA Manowari ya Kijeshi ya Kimerikani USS CORONADO (AGF-11) iliyozuru Mombasa hivi karibuni walitoa zawadi na vifaa mbali mbali kwa shule, hospitali na makao ya walemavu wakati wa ziara yao. Pichani wanamaji Robert L. Holdredge na William R. Walls Jnr. wanaonekana wakipeana zawadi za nguo kwa mwalimu mkuu wa shule ya viwete Port Reitz Bw. Mbaru akiwa pamoja na wanafunzi wake. PICHA: FRED KLINKENBERGER JR.

COASTWEEK

JISHINDIE

Miavuli maridadi katika shindano jipya la kujaza

SWAHILI CROSSWORD NO. 124



JINA ....

SANDUKU LA POSTA ....

KWENDA KULIA:

1. Samaki mkavu wa kuanikwa.
5. Pevuka, komaa.
7. Yaambiwa kuwa.
8. Mchezo wa ngumi.
9. Ndani kwa Kimombo.
10. Sehemu muhimu katika jicho.
11. Bila kula hata karata moja katika mchezo wa karata.
11. Aina ya samaki wa bahari.
12. Hewa.
13. Moyo.
14. Washa.
15. Kanya, kataza.
16. ...... mbele mauti nyuma.

KWENDA CHINI:

1. Wingi wa neno wangwa.
2. Bembeleza.
3. Chagua moja moja ukiweka kando.
4. Karata yenye chapa ya bibi, mke.
6. Jinsi, namna.

Washindi wa Fumbo la Kujaza Maneno No. 123

1] Edward Mutahi, Sanduku la Posta 90352, Mombasa.

2] Richard N. Kinga, Sanduku la Posta 93100, Changamwe.

3] Ermintrude Njeri, Sanduku la Posta 96112, Likoni, Msa.

Washindi waombwa wafike afisini mwa COASTWEEK.

MAJIBU YA SHINDANO LA FUMBO LA KUJAZA MANENO NO. 123 —

KWENDA KULIA:

1. KONGOWEA, 5. NDAMA, 7. EWE, 8. AM, 10. UKAME, 12. DONDA, 13. UK, 14. JINA, 15. TUMBA, 16. FUA, 17. AGUA.

KWENDA CHINI:

1. KINANDA, 2. GOMA, 3. ELEZA, 4. TELEKA, 6. AMUA, 9. UNGUA, 11. MUNDU, 14. JAA, 15. TU.

Shindano la Fumbo la Kujaza Maneno:

Uamuzi wa majaji utakuwa wa mwisho. Hakuna malalamiko yoyote yatakayo kubaliwa.

Washindi watatu kila baada ya wiki mbili watapata miavuli maridadi. Shindano hili limedhaminiwa na COASTWEEK LIMITED, Mombasa.

Jawabu za Fumbo hili lipelekwe kwa Muhariri, COASTWEEK, Sanduku la Posta 87270, Mombasa, Kenya. Siku ya Jumatano tarehe 26.8.81 saa nne asubuhi shindano hili litakuwa mwisho.